**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

KAMATI YA KUDUMU YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

Idara ya Kamati za Bunge,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA.**

**29 MEI, 2025**

**YALIYOMO**

*Ukurasa*


**YALIYOMO** ..... i
**ORODHA YA VIELELEZO** ..... ii
**SEHEMU YA KWANZA** ..... 1
1.0 **UTANGULIZI** ..... 1
1.1 Maelezo ya Jumla ..... 1
1.2 Msingi wa Uchambuzi ..... 2
1.3 Mawanda ya Taarifa ..... 3
**SEHEMU YA PILI** ..... 4
2.0 **UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025** ..... 4
2.1 Maelezo ya Jumla ..... 4
2.1.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati ..... 5
2.1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha ..... 6
2.1.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara ..... 12
2.1.4 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ..... 13
2.1.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina ..... 15
**SEHEMU YA TATU** ..... 19
3.0 **UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ..... 19
3.1 Makadirio ya Mapato ..... 19
3.2 Makadirio ya Matumizi ..... 21
3.3 Mambo muhimu yanayogusa Sekta ya ardhi ..... 24
**SEHEMU YA NNE** ..... 28
4.0 **MAONI YA USHAURI** ..... 28
4.1 Maoni ya Jumla ..... 28
4.2 Ushauri wa Kamati ..... 28
4.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli ..... 28
4.2.2 Mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi (KKK) ..... 29
4.2.3 Mfumo Unganishi wa Kielekroniki wa Huduma za Ardhi (e-Ardhi) ..... 29
4.2.4 Changamoto ya Ukosefu wa wakaguzi majengo nchini ..... 30
4.2.5 Ucheleweshaji wa Fidia ya Ardhi katika Maeneo yaliyofanyiwa Uthamini ..... 30
4.2.6 Migogoro ya Ardhi Nchini ..... 30
4.2.7 Wawekezaji wakubwa katika Sekta ya Ardhi ambao Hawajaendeleza Maeneo yao ..... 31
4.2.8 Ufinyu wa Bajeti katika Tume ya Taifa ya mipango ya ardhi ..... 31
**SEHEMU YA TANO** ..... 32
5.0 **HITIMISHO** ..... 32

# ORODHA YA VIELELEZO

**Ukurasa**

**Kielelezo Na. 1:** Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2025 .......................... 15
**Kielelezo Na. 2:** Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 48 .......................................... 16
**Kielelezo Na. 3:** Upatikanaji wa Fedha (Fungu 03) ............................................... 18
**Kielelezo Na. 4:** Mchanganuo wa makadirio ya Maduhuli ................................ 21
**Kielelezo Na. 5:** Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mwaka 2025/2026 - Fungu 48 ................. 22
**Kielelezo Na. 6:** Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka 2025/2026 - Fungu 03 ................. 23

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,Toleo la Februari,2023 {Kanuni za Bunge},naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi,Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (5) kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza inayotoa, Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inahusu Uchambuzi wa tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na
(iii) Sehemu ya tatu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2025/2026;
(iv) Sehemu ya nne inayohusu Maoni Ushauri; na
(v) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii umejengwa katika Masharti ya Kanuni za Bunge ambapo Kifungu cha 6(8)(a)(b) kikisomwa kwa Pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari,2023, kinaitambua Kamati hii kuwa na wajibu wa kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara hii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.Katika hatua hiyo Kamati ilifanya uchambuzi wa

kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

## 1.3 Mawanda ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo: -

(i) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

**Mheshimiwa Spika**, mambo yaliyochambuliwa yalijitokeza katika randama ya Mpango na Bajeti ya **Fungu 48** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na randama ya Mpango na Bajeti ya **Fungu 03** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.Wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia na uwiano. Aidha, njia iliyotumika ni tathmini ya Jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali ambapo mambo hayo yaliiwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo ilizitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, tarehe 20 – 21 Machi, 2025, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo ilijumuisha Mpango na Bajeti ya Wizara **Fungu 48** pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **Fungu 03.**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;
(ii) Ukaguzi wa Miradi;
(iii) Utekelezaji wa Vipaumbele;
(iv) Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli; na
(v) Hali ya upatikanaji wa Fedha.

### 2.1.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge lilipojadili Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 tarehe 24 na 27 Mei,2024, Kamati ilitoa ushauri katika mambo saba (07) kwa **Fungu 48** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa maeneo mahsusi mawili (2) kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **(Fungu 03).** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa baadhi ya maeneo ushauri wa Kamati umezingatiwa huku maeneo mengine utekelezaji wa ushauri wa kamati haujafanyiwa kwa kiwango cha kuridhisha

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu kuongeza watumishi wa sekta ya ardhi nchini ili kupunguza uhaba wa watumishi katika sekta hiyo. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilifanikiwa kuajiri watumishi 197 wa kada mbalimbali katika sekta za ardhi nchini. Aidha, katika mwaka 2024/2025 Wizara imepata kibali cha kuajiri watumishi 34 ambapo Kamati inaitaka Wizara kuajiri wakaguzi wa majengo (**inspector building**) kwa ajili ya kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kudhibiti ujenzi holela nchini.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika urejeshwaji wa fedha za mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK), Kamati inapenda kulijulisha Bunge kuwa utekelezaji wa azimio hili unaendelea kufanyiwa kazi. Hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2025 fedha zilizorejeshwa ni shilingi **bilioni 29.1** kutoka

shilingi **bilioni 22.4** zilizokuwa zimekusanywa katika kipindi cha Machi, 2024 ikiwa ni ongezeko la takribani **asilimia 30** ya marejesho. Aidha, Halmashauri zilizomaliza marejesho zimeongezeka kutoka Halmashauri **12** hadi kufikia Halmashauri **20**. Kamati inaitaka Wizara kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa na kufanya mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi nchini kuwa endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, kuna maeneo ambayo utekelezaji wa ushauri wa Kamati hauridhishi ikiwa ni pamoja na ukusanyaji hafifu wa madeni ya pango la nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Taarifa ya Wizara inaonyesha kuwa Shirika limekusanya takribani Shilingi **milioni 300** ikiwa ni **asilimia 14.3** ya madeni yote inayodai. Kamati imebaini kuwa Shirika halina mpango madhubuti wa ufuatiliaji wa madeni ya kodi ya pango la nyumba. Hali hii inaweza kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa ufanisi kwani fedha hizi ni moja ya chanzo kikuu cha mapato kwa shirika.

### 2.1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya miradi ya maendeleo hupitishwa na Bunge kwa lengo la kuimarisha sekta inayohusika ili kutoa mchango katika kukuza Uchumi na kuleta ustawi wa maendeleo ya wananchi. Kwa vile Bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linahitaji kujiridhisha

na hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoidhinishiwa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, tarehe 12 hadi tarehe 19 Machi, 2025, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mitatu (03) inayotekelezwa katika mikoa miwili ambayo ni Manyara na Kilimanjaro. Miradi hiyo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha **Shilingi 70,656,510,000** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Naomba kubainisha na kufafanua miradi hiyo pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo: -

**(a) Mradi Namba 2326: Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) katika halmashauri ya Mji wa Babati**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kwa uratibu wa Wizara rya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kutoa mikopo ya fedha isiyo na riba kwa halmashauri nchini. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi **cha Shilingi 4,026,000,000** kwa ajili ya kutekeleza mradi huu kwenye halmashauri mbalimbali nchini. Kamati ilitembelea na kukagua utekelezji wa mradi wa **KKK** kwenye mitaa ya Sawe na Nangara katika Halmashauri ya Mji wa Babati Mkoani Manyara.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Mji babati ilipatiwa na Wizara mkopo usio na riba kiasi **cha Shilingi 250,000,000/=.** Halmashauri ilitekeleza mradi huu kupitia kampuni mbili za upimaji ambazo ni Land General Planning Co.LTD na Kampuni ya Millenium Surveyors na kufanikiwa kupima viwanja **3969** kwa ajili makazi, biashara, viwanda, huduma na miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** na halmashauri inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 476,280,000/=** kupitia mradi huu. Aidha, mradi huu utainufaisha halmashauri kwa kuingizia mapato kiasi cha **Shilingi 226,280,000** kama faida baada ya kurejesha fedha za mkopo kiasi cha **Shilingi 250,000,000/=** ambazo zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Kamati inatembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu tarehe 12 Machi, 2025, halmashauri ilikuwa imefanikiwa kukusanya na kurejesha kiasi cha **Shilingi 103,717,091/=** sawa na **asilimia 41** ya fedha inayotakiwa kurejeshwa. Hata hivyo, Kamati ilitarifiwa kuwa zoezi la uuzaji wa viwanja na kutolewa kwa hati linaendelea miongoni mwa wananchi na halmashauri imepanga kutumia

sehemu ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni liliobakia.

(b) **Mradi Namba 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Tume iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 5,041,232,000/=** kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa kuandaa matumizi ya ardhi katika vijiji 24 kati ya vijiji 68 kwenye Halmashauri ya Willaya ya Rombo tarehe 15 Machi, 2025. Mradi huu ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 ukurasa wa 120 ambapo katika Ibara ya 74, inataka Serikali kupanga matumizi ya ardhi katika vijiji vilivyo katika wilaya za mipakani.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** ambapo Kamati ilishiriki katika utoaji wa Hati Miliki za Kimila ishirini na moja **(21)** kwenye kijiji cha Kisale Msaranga. Aidha, Kamati ilishuhudia hatua mbalimbali katika utatuzi wa migogoro ikiwa ni matokeo ya utekelezaji wa zoezi la upangaji wa matumizi ya ardhi katika kijiji eneo la mradi.

(c) **Mradi wa Kandarasi ya Ujenzi wa Soko la Madini Unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Wilaya ya Simanjiro**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linatekeleza Kandarasi ya ujenzi wa Soko la Madini katika Wilaya ya Simanjiro. Aidha, mteja katika mradi huo ni Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro na unatekelezwa kwa kiasi cha **Shilingi 5,494,724,533.28.** Katika mkataba wa awali, mkandarasi alitakiwa kufanya usanifu na kujenga (design and build) sakafu 3 yaani (G plus 2). Hata hivyo, kufuatia mahitaji ya soko hilo kuwa makubwa, mkataba ulibadilishwa na Shirika kuongezewa kazi ya kujenga jengo la sakafu 5 yaani (G plus 4).

**Mhemiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua mradi huo ambapo ilibaini kuwa mradi umefikia **asilimia 98** kwa mkataba wa awali. Changamoto kubwa katika utekelezaji wa mradi huu ni upatikanaji wa fedha kwa wakati kwani uwezo wa halmashauri katika kufanya malipo ni mdogo. Kamati inalitaka Shirika kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kufanikisha malipo kwa ajili ya kumalizia sehemu ya utekelezaji wa mradi.

**Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa za utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa pamoja na hali halisi iliyobainika wakati wa ziara, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati imefikia hatua nzuri na hali inayoonesha kuwa miradi hiyo itakamilika kwa wakati na mengine ikiwa imefikia asilimia 100;

(ii) Wakati wa utekelezaji wa miradi, Wizara na Tume ziliwashirikisha wadau na wanachi ambao ni wanufaika wa miradi husika; na

(iii) Kasi ndogo ya wananchi katika kulipia viwanja hati ya viwanja vilivyopimwa kupitia mradi wa Kupanga, Kupima
na Kumilikisha Ardhi (KKK).

**Mheshimwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Wizara kwa miradi iliyokamilika ianze kutoa huduma na kwa ile ambayo haijakamilika Wizara iongeze usimamizi.

### 2.1.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 20 Machi, 2025 Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka wa Fedha 2024/2025. Wakati wa uchambuzi wake Kamati ilizingatia vipaumbele vya wizara ambavyo ni: -

(i) Kukamilisha kanuni na miongozo ya uendelezaji wa milki;
(ii) Kutoa elimu ya sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa uendelezaji miji katika Ofisi za ardhi;
(iii) Kufanya tafiti kuhusu makzi yasiyo rasmi;
(iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya urasimishaji na kuzuia makazi yasiyo rasmi;
(v) Kutoa elimu kwa wadau wa sekta ya ardhi katika mikoa 26 kuhusu matumizi ya Mfumo unganishi wa Taarifa za Ardhi (e-Ardhi);
(vi) Kuratibu na kusimamia mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni katika sekta ya ardhi nchini;
(vii) Kufanya Ukaguzi wa uzingativu wa Mipango ya matumizi ya Ardhi iliyoandaliwa katika vijiji;
(viii) Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi; na
(ix) Kufanya tafiti kuhusu makazi yasiyo rasmi

**Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kufanya baadhi ya shughuli ili kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea. Baadhi ya Shughuli hizo ni pamoja na: -

(i) Kufanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 (Toleo la Mwaka 2023). Zoezi hilo limekamilika na kuzinduliwa rasmi tarehe 17 Machi,2025;

(ii) Upimaji wa maeneo kwa kutumia picha za anga katika maeneo ya Ndachi na Chamwino mkoani Dodoma na uwanja wa michezo AFCON 2027 Jijini Arusha;

(iii) Kuanza Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000;

(iv) Kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya vijiji 280 katika maeneo yaliyopitiwa na miradi ya kimkakati na maeneo ya vijiji vya mpakani.

### 2.1.4 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** kama sehemu ya msingi katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara, Kamati ilipokea taarifa ya Serikali kuhusu hali ya ukusanyaji wa maduhuli kwa **Fungu 48 na Fungu 03**. Katika uchambuzi wake, Kamati ililenga kulisaidia Bunge kupata uhalisia na taswira kamili kuhusu uwezo wa Wizara katika ukusanyaji maduhuli. Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia masuala yafuatayo: -

(i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo; na

(ii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Fungu 48** ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 250,000,000,000/=.** Hadi kufikia Februari, 2025 wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 110,322,568,159.57** sawa na **asilimia 44.13** tu ya lengo la makadirio ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti ambao ni **asilimia 66.7.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, uwezekano wa Wizara kufikia lengo la ukusanyaji ni mdogo kwani katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo makusanyo ya wizara yamekuwa chini asilimia 60 ya lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **(fungu 03**) ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 1,018,000,000/=**. Hadi kufikia Februari,2025, Tume ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 497,755,055/=** sawa na **asilimia 48.90** tu ya lengo ikilinganishwa na muda wa utekelezaji wa bajeti ambao umefikia **asilimia 66.7**. Kamati inaitaka Wizara kuongeza usimamizi kwenye Tume ili iweze kufikia malengo ya makusanyo kama ilivyotarajiwa.

**Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2025**

| Fungu | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Wizara(48) | 250,000,000,000.00 | 110,322,568,159 | 44.13 |
| Tume(03) | 1,018,000,000.00 | 497,755,055 | 48.90 |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara, 2025 ana Usanifu wa Kamati*

### 2.1.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara unategemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 48 na Fungu 03 kutoka hazina kama ifuatavyo: -

**(a) Fungu 48: Wizara ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 48 hadi kufikia mwezi Februari, 2025 umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Fedha za matumizi ya kawaida zilipatikana kwa **asilimia 54** ikiwa ni upungufu wa fedha zilizotakiwa katika kipindi kama hicho kwa **asilimia 12.7**

(ii) Katika kiasi hicho cha fedha za kawaida fedha za matumizi mengineyo **(OC)** zilikuwa **asilimia 47** ya fedha zote huku mshahara ikiwa imepatikana kwa **asilimia 60;**

(iii) Fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa **asilimia 76** ya bajeti; na

(iv) Katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo, fedha za Ndani zilifikia **asilimia 91** na fedha za nje **asilimia 63**. Hata hivyo, katika fedha za ndani **asilimia 77.5** ilikuwa ni fedha ya kulipia madeni mbalimbali ya Wizara.

**Kielelezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 48**

| AINAYA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mshahara | 50,155,528,000 | 29,897,974,318 | 59.61 |
| Matumizi Mengineyo | 36,643,047,000 | 17,402,708,975 | 47.49 |
| JUMLA (A) | 86,798,575,000 | 47,300,683,293 | 54.49 |
| Miradi ya maendeleo | 70,656,510,000 | 48,491,806,442 | 68.63 |
| Kulipa madeni ya Serikali | 36,508,813,000 | 36,508,813,000 | 100 |
| JUMLA | 107,165,323,000 | 85,000,619,442 | 79.32 |

**Mheshimiwa Spika,** kupitia kielelezo **Na. 2** ni wazi kuwa Wizara imepokea fedha za kutosha katika utekelezaji wa majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye vipaumbele vyake. Kamati inaitaka Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwani Serikali imetoa fedha kwa wakati na kuzingatia umuhimu wa shughuli za Wizara.

## a) Fungu 03: Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**), uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2025 ulionesha mambo yafuatayo: -

(i) Tume ilipokea **asilimia 58.8** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo;

(ii) Fedha za matumizi ya Kawaida zilizopokelewa zilikuwa **asilimia 55.46** ya bajeti yote;

(iii) Katika kiasi hicho cha fedha za matumizi ya kawaida, Fedha za matumizi mengineyo **(OC)** zilipokelewa kwa **asilimia 50.3** na huku mishahara ikiwa imepokelewa kwa **asilimia 59.7;**

(iv) Fedha za miradi ya Maendeleo zilipokelewa kwa **asilimia 63.59** huku fedha zote zikiwa fedha za ndani. Taswira halisi ya mwenendo wa fedha inaonekana katika **Kielelezo Na.03.**

### Kielelezo Na. 3: Upatikanaji wa Fedha (Fungu 03)

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 3,887,780,000 | 2,321,089,000 | 59.7 |
| Matumizi Mengineyo (0C) | 3,244,318,000 | 1,634,467,833 | 50.3 |
| Mradi wa Maendeleo | 5,041,232,000 | 3,205,722,500 | 63.59 |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizar ana usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa upatakinaji wa fedha hauridhishi kwani kiasi kilichopokelewa ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotakiwa kupelekwa kwenye Tume toka Serikalini katika kipindi hicho. Hali hii inaweza kupelekea Tume kushindwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyotarajiwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia masharti ya kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026;
(ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na
(iii) Mambo muhimu yanayogusa sekta ya ardhi.

### 3.1 Makadirio ya Mapato

**a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa kuhusu lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi ulijikita zaidi kwa kuangalia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inakadiriwa kukusanya maduhuli ya Shilingi **265,000,000,000/=**. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa makadirio hayo yameongezeka kwa **shilingi 15,000,000,000** sawa **asilimia 6** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa pamoja na kuongezeka kwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli ni dhahiri kuwa malengo hayo hayawezi kufikiwa. Hii inatokana na ukweli kuwa mwenendo wa makusanyo kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo unaonesha kuwa, Wizara ilishindwa kufikia hata **asilimia 50** ya ukusanyaji wa maduhuli yaliyoidhinishwa.

**b) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **Fungu 03** inakadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,018,000,000**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa lengo la makusanyo katika mwaka wa fedha 2025/2026 linalingana na lile la mwaka wa fedha 2024/2025.

**Kielelezo Na. 4: Mchanganuo wa makadirio ya Maduhuli**

| FUNGU | Mwaka 2024/2024 | Mwaka 2025/2026 | Ongezeko/ punguzo | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wizara (48) | 250,000,000 | 265,000,000,000 | 15,000,000,000 | 6 |
| Tume (03) | 1,018,000,000 | 1,018,000,000 | 0 | 0 |

## 3.2 Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo: -

a) **Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu – 48)**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 153,437,867,000** ili kuimarisha sekta za ardhi na nyumba nchini. Matokeo ya uchambuzi katika makadirio ya matumizi ya fedha hizo yanaonyesha kuwa: -

(i) Jumla ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeshuka kwa **asilimia 2.6** ikilinganishwa na ya mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Shilingi**

**4,581,463,000** sawa na **asilimia 5.3** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeshuka kwa kiasi cha **Shilingi 8,598,681,000** sawa na **asilimia 12.2** ikilinganishwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Taswira ya makadirio ya matumizi kwa **Fungu 48** wizara inaonekana katika **Kielelezo Na. 5**

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mwaka 2025/2026 - Fungu 48**

| AINA YA MATUMIZI | MWAKA 2024/2025 | MWAKA 2025/2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 50,155,528,000 | 53,820,915,000 | 6 |
| Matumizi mengineyo | 36,643,047,000 | 37,559,123,000 | 2.5 |
| **JUMLA** | **86,798,575,000** | **91,380,038,000** | **5.3** |
| Miradi ya Maendeleo | 70,656,510,000 | 62,057,829,000 | 12.2 |
| **JUMLA KUU** | **157,455,085,000** | **153,437,867,000** | **2.6** |

**b) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu – 3).**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Tume,** inakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 10,708,185,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ili kuleta ustawi wa wananchi katika matumizi bora ya ardhi nchini. Kamati imechambua na kubaini kuwa: -

(i) Jumla ya bajeti kwa Fungu 03 imepungua kwa kiasi cha **Shilingi 1,465,145,000** sawa na **asilimia 12 .04** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **Shilingi 1,055,471,000** sawa na **asilimia 14.8** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imepungua kwa kiasi cha **Shilingi 2,520,616,000** sawa na **asilimia 50** ikilinganishwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Taswira ya makadirio ya matumizi kwa **Fungu 03** Tume ya matumizi ya ardhi inaonekana katika **Kielelezo Na. 6**

**Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka 2025/2026 - Fungu 03**

| AINA YA MATUMIZI | MWAKA 2024/2025 | MWAKA 2025/2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 3,887,780,000 | 4,712,143,000 | 21 |
| Matumizi Mengineyo | 3,244,318,000 | 3,475,426,000 | 7 |
| **JUMLA** | **7,132,098,000** | **8,187,569,000** | **14.8** |
| Miradi ya Maendeleo | 5,041,232,000 | 2,520,616,000 | 50 |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizara ya Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitika kuona kuwa matumizi ya fedha za maendeleo yamepungua kwa

takribani asilimia 50 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2024/2025. Hali hii inatoa tasfiri kuwa, katika mwaka ujao wa fedha, Tume inatarajiwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo machache zaidi. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaongeza fedha za maendeleo ili kuiwezesha Tume kutekeleza zoezi la kuandaa Mipango ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo mengi zaidi.

### 3.3 Mambo muhimu yanayogusa Sekta ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kujadili mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilibaini mambo muhimu yanayogusa Wizara hii kama ifuatavyo: -

(a) **Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK).**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa ya Serikali kuhusu mradi huu ambapo ilibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilipanga kutekeleza Programu hii kwa kutumia Mfuko wa Plot Development Revolving Fund (PDRF). Katika program hii Wizara ilipanga kupima na kutoa Hati za Kumiliki Ardhi **100,000** (CRO) za viwanja vipya na vya Urasimishaji ifikapo Juni, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepima viwanja **8,049** katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, taarifa ya Wizara kuhusu mradi huu inaonesha kuwa Vifaa vya kuandalia hati vimenunuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, kasi ya utekelezaji wa mradi wa KKK ni ndogo sana kulinganisha na lengo lililokusudiwa. Wizara imeweza kupima **asilimia 8.05** tu ya viwanja vilivyopangwa hadi kufikia Februari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inaongeza kasi katika utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi ili kuweza kufikia lengo walilokusudiwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025

(b) **Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).**

Ibara ya 76 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 iliitaka Serikali Kuendelea kuboresha na kuimarisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Pamoja na majukumu mengine, Shirika lilitakiwa kukamilisha ujenzi wa nyumba za majengo makubwa ikiwemo Morocco Square, Kawe 711, Golden Premier Residence na Mradi wa Kiwanja Na. 300 Regent Estate katika jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika linaendelea na ujenzi wa nyumba 422 katika mradi wa Kawe 711 unaotarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2026. Vilevile, Shirika lipo katika mchakato wa kufanya upembuzi yakinifu na manunuzi katika ujenzi wa nyumba 196 katika mradi wa Golden Premium Residence (GPR) na Kiwanja namba 300 Regent Estate ambapo ujenzi wake unategemea kuanza ndani ya mwaka ujao wa fedha. Kamati

inaitaka Serikali kuhakikisha inashughulikia changamoto ya wakandarasi na Shirika ili miradi hiyo itekelezwe kwa ufanisi.

(c) **Migogoro ya Ardhi Nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi katika nchi yetu haswa ya wanachi kumavamia maeneo ya Taasisi za Serikali, mashamba ya Serikali na hata ya maeneo ya watu binafsi. Hali hii inapelekea kuzalisha migogoro kati ya Serikali na *wananchi, na wananchi na wananchi.*

**Mheshimiwa Spika,** kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali katika kutatua migogoro hiyo hata hivyo kamati inaishauri Wizara kuweka mpango madhubuti wa kukabiliana na migogoro hiyo ili isiwe ya kujirudia na kuepusha madhara yanayotokana na migogoro hiyo ikiwa ni uvunjifu wa amani na kukwamisha shughuli za uzalishaji.

(d) **Ulipaji wa Fidia ya Ardhi kwenye maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya Miradi ya Serikali na Uwekezaji.**

**Mheshimiwa Spika,** Fidia ni malipo yanayotolewa kwa mtu au taasisi kama mbadala wa mali yake au kutokana na kuondolewa kwenye eneo lake linalotwaliwa kwa manufaa ya umma au kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa. Ili

kukadiria kiasi cha fidia kitakacholipwa kwa mwananchi ambaye mali zake zimetwaliwa kwa manufaa ya umma, sheria inaelekeza kuwa thamani ya mali hizo zinapaswa kukadiriwa na mthamini aliyesajiliwa na bodi ya wathamini.

**Mheshimiwa Spika,** katika ulipaji wa fidia hiyo, Kamati imebaini kuwa kuna changamoto ya ucheleweshaji wa malipo ya fidia kwenye maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili matumizi mbadala. Uchelewashaji wa malipo ya fidia unatokana na zoezi la uhakiki (financial verification) kuwa la muda mrefu na kukosekana kwa fedha katika mfuko wa Fidia ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka ili kuondoa changamoto hii. Aidha, Serikali ihakikishe kabla ya kufanya uthamini wa ardhi inakuwa na fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi watakaokuwa wametwaliwa maeneo yao.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI YA USHAURI

### 4.1 Maoni ya Jumla

(i) Wizara iongeze jitahada za kuweza kupima na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vyote ili kuondoa migogoro ya ardhi nchini;

(ii) Wizara ihakikishe inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama yalivyopangwa kwenye bajeti; na

(iii) Wizara ihakikishe inasambaza Mfumo Unganishi wa Kielektroniki wa huduma za Ardhi (e-ardhi) katika Mikoa yote nchini.

### 4.2 Ushauri wa Kamati

#### 4.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwani Wizara hii imekuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji;

(ii) Irejeshe utaratibu wa kodi ya pango la ardhi (Land Rent) kukusanywa na Wizara ambayo ndio ina nyenzo za kisheria na mifumo ya ukusanyaji wa kodi hiyo; na

(iii) Iihakikishe inatengeneza mipango na mbinu za kufuatilia wadaiwa wa pango la ardhi ili kuweza kuongeza mapato ya Wizara.

### 4.2.2 Mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi (KKK)

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iongeze kasi ya Kupanga na kupima ili kufikia lengo la viwanja 100,000 hadi kufikia Juni, 2025;

(ii) Ihakikishe Wizara inashirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhimiza wakurugenzi wa halmashauri ambazo hazijarejesha fedha hizo kurejesha fedha hizo ili kufanya proramu ya KKK kuwa endelevu katika halmashauri zote nchini;

(iii) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu manufaa ya kumiliki ardhi kwa njia rasmi hali itakayochochea wananchi wengi kulipia hati za umiliki wa maeneo yaliyopimwa kupitia mradi wa KKK; na

(iv) Iongeze idadi ya wasimamizi wa mradi ili kuongeza ufanisi wa programu hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.

### 4.2.3 Mfumo Unganishi wa Kielekroniki wa Huduma za Ardhi (e-Ardhi)

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe inaongeza kasi ya kusambaza Mfumo wa e-Ardhi kwenye halmasahuri zote nchini ili shughuli zote za Ardhi zifanyike kwenye mifumo;

(ii) Ihakikishe inafanya maboresho ya mfumo ili uwe rafiki kwa watumiaji;na

(iii) Ihakikishe inatoa elimu kwa Maafisa ardhi na wananchi wote kuhusu Mfumo wa utoaji huduma katika usimamizi wa Ardhi.

### 4.2.4 Changamoto ya Ukosefu wa wakaguzi majengo nchini

Kamati inashauri Serikali kuwa ihakikishe inaajiri wakaguzi majengo katika Halmashauri zote ili kuzuia ujenzi holela nchini;

### 4.2.5 Ucheleweshaji wa Fidia ya Ardhi katika Maeneo yaliyofanyiwa Uthamini

Kamati ianashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe inakuwa na fedha kabla ya kuanza zoezi la kufanya uthamini na mchakato wa utwaaji wa ardhi ya wananchi;

(ii) Ifanye marekebisho ya Sheria kwa ajili ya kuufanya mfuko wa fidia ya ardhi nchini kuwa chini ya mthamini Mkuu wa Serikali.Hali itakayomfanya mthamini mkuu wa Serikali kujua uwezo wa mfuko kabla ya kwenda kufanya uthamini.

### 4.2.6 Migogoro ya Ardhi Nchini

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe kuwa inakuwa na kanzidata ya maeneo yote yaliyopangwa na kupimwa ili kuwezesha wananchi kufanya ujenzi wa makazi kwenye maeneo rasmi nchini;

(ii) Ihakikishe inaandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuondaoa migogoro inayojitokeza hapa nchini; na

(iii) Ihakikishe Clinic za Ardhi zinakuwa endelevu na zifanyike kwa mikoa yote ili kuendelea kupunguza migogoro ya ardhi.

### 4.2.7 Wawekezaji wakubwa katika Sekta ya Ardhi ambao Hawajaendeleza Maeneo yao

Kamati inasahuri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe inafanya tathimini ya wawekezaji katika sekta ya ardhi nchini ili kutambua hali ya uendelezaji wa maeneo hayo; na

(ii) Ichukue hatua kwa wawekezaji ambao wameshindwa kuendeleza maeneo yao kwa kuzingatia Sheria.

### 4.2.8 Ufinyu wa Bajeti katika Tume ya Taifa ya mipango ya ardhi

Kamati inashauri Serikali kuwa, iongeze fedha za maendeleo ili kuiwezesha Tume kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji vingi nchini.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya kamati napenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu katika kulisimamia na kuliwezesha Bunge letu kutekeleza wajibu wake wa kusimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza na kumshukuru sana **Mhe Deogratius John Ndejembi (Mb),** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mhe.Geophrey M. Pinda (Mb) Naibu Waziri kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara chini ya Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga, Naibu Katibu Mkuu Ndg.Lucy Kabyemela kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na usimamizi mzuri wa majukumu ya wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee nawapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa waliofanya hadi taarifa hii inaingia Bungeni. Majina ya wajumbe hao yameorodheshwa katika taarifa hii ila kwa sababu ya changamoto ya muda naomba majina yao yaingie kwenye taarifa rasmi za Bunge yaani hansard.

Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Timotheo P. Mnzava, Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Askofu Josephat M. Gwajima, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Neema William Mgaya, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Innocent Bilakwate, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Dkt Florence G. Samizi, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Festo Richard Sanga, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Shaban Omari Shekilindi, Mb | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Asha Juma Abdallah, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, naomba nimalize kwa kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini

ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Timotheo P. Mnzava, Mb

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

29 Mei, 2025